The University of Osaka
Institutional Knowledge Archive

| | |
|---|---|
| Title | Utamaduni wa Kiswahili: Fasihi na Sanaa Nyingine |
| Author(s) | Isack, Zainabu Kass |
| Citation | 外国語教育のフロンティア. 2025, 8, p. 65-78 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/100884 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Utamaduni wa Kiswahili: Fasihi na Sanaa Nyingine

## Swahili Culture: Literature & Other Forms of Art

ISACK, Zainabu Kassu

**Ikisiri**

Makala hii fupi ni sehemu ya mfululizo wa makala juu ya Utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla. Mara hii tumelenga kufanunua Fasihi ya Kiswahili sambamba na vipengele vingine vya Sanaa chini ya mada Utamaduni wa Kiswahili: Fasihi na Sanaa Nyingine. Kama tujuavyo Fasihi ni kipengele kimojawapo cha sanaa lakini tumekipa uzito katika mjadala wa mada husika kutokana na utofauti wake na sanaa nyingine na umuhimu wake kama sehemu ya utambulisho wa utamaduni wa watu. Kama ilivyo kwa makala tulizotangulia kuchapisha katika mfululizo huu; Maudhui tajwa yanatarajiwa kuwanufaisha wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni katika kutajirisha maarifa yao na kuziba mwanya wa rejea zinazowalenga kundi hili juu ya lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla wake.

Keywords: Fasihi ya Kiswahili, Sanaa

**Abstract**

This brief article continues our series on Swahili and African culture. Titled “Swahili Culture: Literature and Other Forms of Art,” it offers a concise overview of this aspect of Swahili culture. Consistent with the author’s earlier works, this content is tailored to aid both instructors and learners of Swahili as a foreign language deepen their understanding of Swahili Culture and African Culture at large.

Keywords: Swahili Literature, art

### 1. Utangulizi

Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu 4: Sehemu ya 1 ni Utangulizi; ambayo inafafanua mpangilio wa makala na lengo la makala. Sehemu ya 2 na 3 ni kiini cha makala hii ambamo tunatolea ufafanuzi juu ya Fasihi kwa upande mmoja na Sanaa nyingine kwa upande mwingine. Ama kuhusu Fasihi; katika sehemu ya 2 tunaeleza mambo ya msingi kuhusiana na Fasihi ya Kiswahili mambo hayo ni pamoja na; dhana ya fasihi kwa ujumla, aina, tanzu, chimbuko na dhima ya fasihi zamani na hata sasa tukirejelea muktadha wa Fasihi ya Kiswahili hususan kutoka katika jamii ya Tanzania. Kwa upande wa Sanaa vile vile katika sehemu ya 3 tunabainisha vipengele teule vya Sanaa vinavyofungamana na Utamaduni wa Kiswahili na kuvitolea maelezo, mifano ya sanaa mahsusi katika kila kipengele sambamba na kuelezea

dhima/kazi za sanaa husika. Vipengele vitatu vilivyoteuliwa ni; Ususi, uchoraji, na uchongaji. Sehemu ya 4 na ya mwisho ni: Hitimisho; sehemu hiyo inatoa muhtasari wa makala hii pamoja na maoni ya mwandishi.

### 1.1 Lengo la Makala

Makala hii fupi iliyo na kichwa "Utamaduni wa Kiswahili: Fasihi na Sanaa Nyingine" inakusudia kutambulisha na kutolea ufafanuzi wa mambo ya msingi kuhusiana na Fasihi na Sanaa nyinginezo zinazofungamana na Utamaduni wa Kiswahili ikiwa ni sehemu ya mfululizo wa makala zilizoandikwa na mwandishi zinazolenga kutajirisha maarifa na kuziba mwanya wa maarifa na rejea kwa wajifunzaji na wakufunzi wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kutimiza dhamira hiyo, tunatumia maandiko yaliyopo juu ya mada husika, tukijaribu kufafanua kwa lugha yenye uwekevu/iktisadi na nyepesi. Pia tutatolea mifano na matumizi halisi ya sanaa teule mbalimbali katika maisha ya kila siku kutokana na rejea au kulingana na tajriba na uelewa wa mwandishi.

Rejea zinazotumika katika makala hii hasa vitabu, ni zile zinazotumika kwa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari na vyuoni nchini Tanzania. Ni matarajio yetu kuwa maelezo ya dhana, mifano na matumizi ya kazi za sanaa katika muktadha wa Utamaduni wa Kiswahili katika makala hii yatamfaa mwanafunzi mgeni mwenye kujifunza Kiswahili na Utamaduni wake au kumpa mahala pa kuanzia yoyote mwenye raghba ya kuzamia kwa undani katika kipengele fulani cha taaluma ya Fasihi ya Kiswahili na Sanaa nyinginezo zilizogusiwa katika makala hii.

Kama ilivyo ada tunakariri kuwa; mtu anapojifunza lugha ya kigeni anajifunza utamaduni wa lugha husika pia. Hivyo tunahitaji rejea za kutosha zinazoangazia vipengele mbalimbali vya utamaduni wa Kiswahili na utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla zinazowalenga kundi husika (wajifunzaji wageni) katika maandiko ya Kiswahili. Makala zilizotangulia zenye mwelekeo huu ni pamoja na: Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili (Isack 2018:105-118), Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili (Isack 2019: 259-269), Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi (Isack 2020:193-205) Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili (Isack 2021: 223-233) na Utamaduni wa Kiswahili: Misingi ya Lugha (Isack 2022: 247-258).

## 2. Fasihi: Dhana, Aina, Tanzu, Chimbuko na Dhima zake

Katika sehemu hii tutaangalia Fasihi katika kiwango cha kinadharia yaani dhana ya fasihi kwa ujumla kilimwengu na dhana hiyo katika utamaduni na maandiko ya Kiswahili. Pia tunabainisha aina za fasihi, tanzu, na dhima (kazi) yake zamani na hata leo kilimwengu na huku tukitolea mifano mahsusi ya kazi za Fasihi ya Kiswahili.

### 2.1 Dhana ya Fasihi

Mulokozi (1996: 1-3) anatueleza kuwa, neno Fasihi kama tulijuavyo sasa ni istilahi inayotumika sawa na "literature" katika Kiingereza istilahi inayotokana na etimolojia ya kilatini

"littera" neno ambalo kiasili linamaanisha "herufi" au "kuandika". Na hili linatuleta katika mjadala wa muda mrefu miongoni mwa wataalamu wenye mitazamo mbalimbali kuhusiana na dhana hiyo (literature) kote ulimwenguni. Tena Mulokozi (kashatajwa) anazigawa na kuzihakiki fasili za dhana hiyo kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali katika mitazamo mikuu mitano na hapa tutatolea muhtasari maelezo hayo bila kukariri moja kwa moja au kwa mpangilio alioujadili mwandishi huyo. Kwanza ni mtazamo unaoihusisha au unaoifunga Fasihi katika maandishi tu na kutanua wigo wa fasihi kana kwamba kila kilichoandikwa ni fasihi na kubagua kile kisichoandikwa kuwa si fasihi. Mtazamo huo unadai kuwa fasihi ni jumla ya maandishi/ machapisho yote katika lugha fulani. Mtazamo wa pili unadai kuwa Fasihi ni maandishi bora au jamii ya kisanaa yenye manufaa ya kudumu. Mtazamo huu wa pili unaelekea kuelemea katika ubunifu wa fasihi lakini pia unayabana mawanda ya fasihi vile vile kama ni maandishi yaliyo bora pekee. Mtazamo wa tatu ni ule ulioasisiwa na wafuasi wa nadharia ya uumbuji (formalism) ambao nao una dosari kwa kuegemea sana katika fani kuliko maudhui na kuegemeza fasihi katika ushairi zaidi kwa dai kuwa Fasihi ni matokeo ya matumizi ya ukiukaji wa taratibu za matumizi ya lugha ya kawaida kwa lengo la kumvutia au kumuathiri msomaji au msikilizaji. Mtazamo wa nne ni ule kwa mujibu wa mwandishi huyo ulioibuka Afrika ya Mashariki unaodai kuwa "Fasihi ni hisi… zinajifafanua kwa njia ya lugha". Na mwandishi anaukosoa mtazamo huu kwa mantiki kuwa Fasihi inao uwezo wa kuibua hisia lakini Fasihi yenyewe haiwezi kuwa "hisi" na kwamba madai kuwa "fasihi ni hisi" ni mparaganyiko wa mambo yaani kuchanganya fasihi yenyewe, yaelezwayo na fasihi na mtindo wake. Mtazamo wa tano na ambao unaelekea kukubalika na mwandishi huyo na ndio utumikao kama msingi katika taaluma ya Fasihi ya Kiswahili hivi sasa ni kuwa neno Fasihi lina maana ya ufasaha na uzuri wa lugha, na kuitofautisha na istilahi "literature" inayotumika katika Kiingereza iliyojiegemeza zaidi katika maandishi.

Kama msisitizo na kubainisha mwelekeo juu ya dhana "Fasihi" katika Kiswahili (kama ilivyotajwa katika mtazamo wa tano hapo juu) Ameir na wenzie (1981:7) wanatueleza kuwa "Kinachofanya fasihi iwe fasihi si maandishi, bali ni usanii ulioshikamana na dhamira iliyokusudiwa, na itolewayo kwa maneno." Ameir na wenzie (wameshatajwa) wanaendelea kubainisha ya kuwa, " Fasihi, kwa mtazamo huu ni sanaa itumiayo maneno ili kutoa picha halisi ya mwanadamu akiwa maishani mwake; mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha zake, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake".

Kwa mantiki hiyo, msimamo na fasili juu ya dhana ya Fasihi katika makala hii basi ni kuwa Fasihi ni sanaa itumiayo lugha ama ya kusemwa (mdomo) au ya kuandikwa (maandishi) yenye sifa ya uzuri na ubunifu, inayoibua hisia na kusawiri maisha na mazingira ya jamii husika kwa malengo la kufunza, kuburudisha, kuonya, kurithisha amali za jamii n.k. Vile vile ni muhimu kueleza kwamba ijapokuwa tumetoa hoja kuwa nyenzo kuu ya fasihi ni lugha, na ukweli kuwa Fasihi na lugha zina uwiano wa dhima ya mawasiliano, si kila matumizi ya lugha ni fasihi. Fasihi hujipambanua na mawasiliano mengine kwa namna fanani (msanii) inavyoifinyanga na kuisanifu lugha katika kuibua hisia na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira (wasikilizaji

au wasomaji wanaoipokea kazi ya kifasihi) yake. Baadhi ya mbinu za kifasihi zinazotumika ili kuipamba na kuipambanua lugha katika kazi ya kifasihi ni pamoja na matumizi ya tamathali za usemi; sitiari, tashibiha, tasfida, vijembe na kejeli/vinyume. Mbinu nyingine ni kama mizani, mapigo ya sauti na vina (hususan katika ushairi), kuyapa maneno maana ya ziada kwa kuihusisha maana ya msingi na maana mpya inayoendana na ile ya msingi.

Vipengele vya kiubunifu katika lugha ya kifasihi kwa pamoja tunaweza kuviita fani navyo hutegemeana na aina ya utanzu wa kazi husika ima ni ushairi, tamthilia, riwaya, hadithi simulizi n.k. Hapa hatutajadili vipengele hivyo kwa undani kwani ni nje ya mawanda na malengo ya makala hii. Kwa ujumla vipengele hivyo ni pamoja na matumizi ya lugha kifasihi kama ilivyotangulia kutajwa hapo juu, uchoraji wa wahusika, usawiri wa mazingira katika kazi husika/ matayarisho ya jukwaa, msuko wa matukio (hususan katika riwaya), mavazi, miundo na mitindo ya usimulizi n.k. Vipengele vya fani katika kazi ya kifasihi huwa ni chombo cha kubebea ujumbe, kuibua hisia na kumpa mpokeaji taswira halisi kulingana na utanzu wa kazi husika.

### 2.2 Fasihi ya Kiswahili, Aina na Tanzu zake

Katika sehemu hii tunafafanua msimamo wetu juu ya dhana Fasihi ya Kiswahili na kisha tunapambanua aina mbili za Fasihi ya Kiswahili nazo ni Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi na kutolea mifano ya tanzu zake kwa kila aina sambamba na kubainisha mfanano au tofauti baina ya aina hizo mbili za Fasihi.

Tukianzia na dhana ya Fasihi ya Kiswahili, ni dhahiri kumekuwa na mjadala mrefu wa wataalamu wa fasihi juu ya dhana inayohusiana na “Waswahili” au “Kiswahili” na “Fasihi” na majina kama “Fasihi ya Waswahili”, “Fasihi katika Kiswahili”, “Fasihi ya Kiswahili” yameibuliwa kama matokeo ya mijadala kama hiyo. Si mahala pake kuingia kwa undani katika kuihakiki mitazamo hiyo kwa muktadha wa makala hii. Katika makala hii tumechagua kutumia dhana Fasihi ya Kiswahili, na tunaungana na kauli ya Syambo na Mazrui (1992:ix) kama walivyonukuliwa katika Mulokozi (1996:24) kuwa; “… hatuna budi kuichukulia fasihi ya Kiswahili kuwa ni ile iliyoandikwa kwa Kiswahili tu, iwapo inazungumzia utamaduni wa Kiswahili au utamaduni mwingineo. Maadamu fasihi hiyo imetumia lugha ya Kiswahili na imefuata mbinu za ufasaha wa lugha hiyo, basi, kwa fasili yetu, ni Fasihi ya Kiswahili.” Na sababu kubwa na kuafikiana na mtazamo kama huu ni ukweli kuwa lugha ya Kiswahili imeenea katika eneo kubwa la Afrika ya Mashariki na kati, na lugha hiyo ndiyo inayotumika kama lugha ya mawasiliano mapana. Aidha lugha hiyo na fasihi yake imekuwa ni chombo kinachowaunganisha watu tangu zama za ukoloni, baada ya uhuru na hata sasa katika zama hizi za utandawazi.

#### 2.2.1 Fasihi Simulizi

Kama jina linavyodokeza Fasihi Simulizi ni ile inayowasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Ukamilifu wa fasihi simulizi (au sifa zinazoifanya fasihi simulizi iwe fasihi simulizi)

unafungamana au kutawaliwa na fanani (msimulizi), hadhira (wasilikizaji), mahala pa utendaji (mf. Nje ya nyumba kuzunguka moto) na utendaji wenyewe/fani inayotendwa au tukio (shughuli husika ya kijamii) ambalo ndilo muktadha wa kijamii unaohusiana na utendaji wa sanaa kama vile harusi, ibada au kazi fulani. Fasihi simulizi hutambulika kama mali ya jamii, haina mmiliki mmoja na zamani ilihifadhiwa katika kumbukumbu tu (vichwani) na kurithishwa kizazi hata kizazi.

Mulokozi (1996: 33) anatanabahisha kuwa ingawa fasihi simulizi ni kongwe, tumekuwa nayo kwa maelfu ya miaka, lakini kama taaluma imeanza kuchunguzwa na kufundishwa mashuleni hivi karibuni. Na Fasihi ya Kiswahili hususan imeanza kufunzwa katika masomo ya kifasihi miaka ya 1960. Hivyo taaluma hiyo bado ni changa na hakuna rejea, nadharia wala istilahi za kutosha za taaluma hiyo. Pamoja na kuwapo kwa baadhi ya vitabu na makala ambazo zimechangia kueneza maarifa juu ya fasihi simulizi Afrika Mashariki, mwandishi huyo anatoa wito kuwa bado maandishi mengi zaidi yanayotokana na utafiti wa uwandani yanahitajika.

Tanzu za Fasihi simulizi ni anwai na zenye kutofautiana kutoka jamii moja na nyingine. Tanzu za fasihi simulizi pia ni zenye ugiligili (mwingiliano). Kwa mujibu wa Mulokozi (1996: 25-26) tunaweza kuzigawa tanzu hizo katika makundi sita ambayo ni; Mazungumzo, Masimulizi, Maigizo, Ushairi, Semi na Ngomezi (mawasiliano kwa njia ya ngoma kwa midundo inayowakilisha kauli fulani za kimapokeo zenye sifa ya kishairi na kimafumbo katika jamii husika). Mazungumzo yanahusisha vitu kama hotuba, malumbano ya watani, soga na mawaidha. Mifano ya masimulizi ni pamoja na hekaya, visakale, tarihi na visasili. Kwa upande wa semi tuna vipengele kama methali, vitendawili, misimu, mafumbo na lakabu. Maigizo yanajumuisha utendaji wa namna ya kuiga kama vile maigizo ya watoto, maigizo ya misibani, shereheni au maigizo katika nyakati za ibada kama matambiko.

### 2.2.2 Fasihi Andishi

Fasihi Andishi ni fasihi iliyoandikwa katika maandishi, nayo huhifadhiwa katika mtindo wa maandishi, ina mmliki ambaye ni mwandishi na haiwezi kurithishwa tofauti na Fasihi Simulizi. Tanzu za Fasihi Andishi ni Ushairi, Riwaya na Tamthilia.

Tukianza na utanzu wa Ushairi: Mulokozi (1996: 94- 96) anafafanua kuwa wataalamu wa fasihi wa Kiswahili na ulimwenguni hawahitalifiani sana juu ya Ushairi kama sanaa yenye sifa ya kuwa na kauli zenye hisia na ubunifu, mpangilio wenye urari, uwasilishaji wa tajriba, au mawazo ya mtunzi kwa namna ambayo huibua tajriba kama hiyo katika nyoyo za wasomaji/wasikilizaji na kuwa ushairi unatumia lugha ya picha yenye wizani wa sauti. Ama kuhusu ushairi wa Kiswahili wataalamu wa fani ya ushairi wamegawanyika katika matapo mawili; tapo moja ni la washairi wa Kiswahili wa kijadi/kimapokeo ambao wanasisitiza juu ya urari wa vina na mizani kama sifa mojawapo ya ushairi pamoja na sifa nyingine kama vile kuwa ushairi ni wimbo, wenye maneno ya hekima, lugha ya mkato, lugha nzito na wenye hisia. Tapo la pili ni la washairi wa Kiswahili wa Kisasa ambao wanakubaliana na sifa za washairi wa kijadi isipokuwa bila kusisitiza juu ya urari wa vina na mizani. Wataalamu wanaounga mkono tapo la ushairi wa Kiswahili wa kijadi ni pamoja na Amri Abedi na Shaaban Robert. Na wafuasi wa tapo la pili ni

pamoja na Kezilahabi, Mulokozi, Topan, na Kahigi.

Utanzu mwingine wa Fasihi Andishi ni riwaya, nayo inaelezwa kama ni masimulizi ya kubuni, yenye muundo wa usimulizi wa kinathari na wenye mpangilio au msuko fulani wa matukio/ploti (Mulokozi 1996: 139-140). Vile vile Mulokozi anaendelea kunbainisha sifa nyingine za riwaya kuwa ni mfungamano wa visa katika wakati fulani, yenye mawanda mapana wa yale yanayozungumzwa, sambamba na wakati na mahali pa matukio hayo. Pia sifa ya muhimu ya riwaya ni uchangamano katika visa, dhamira na tabia za wahusika. Urefu wa riwaya unapendekezwa kuwa kati ya maneno 35,000 na kuendelea, hata hivyo inatajwa kuwa riwaya nyingi za Kiswahili si ndefu sana; zina wastani wa maneno baina ya 10,000 na 20,000 pengine tungeweza kuziita novela, ijapokuwa baadhi yake zimechangamana kama riwaya ndefu. Riwaya zinaweza kugawanywa katika makundi makuu mawili; riwaya-dhati na riwaya-pendwa. Riwaya-dhati ni zile zinazolenga kuchambua mambo mazito ya kijamii au kimaisha. Na Riwaya-pendwa kwa upande mwingine hulenga kuburudisha. Riwaya za Kiswahili zinasemaekana zimepanuka na kupevuka katika miaka ya 1970 - 1995 na kuwa hapakuwa na riwaya ya Kiswahili kabla ya mwaka 1930, Uhuru wa Watumwa inatajwa kama riwaya halisi ya kwanza ya Kiswahili. Miongoni mwa waandishi mashuhuri wa kazi za riwaya ni pamoja na Shaaban Robert, Euphrase Kezilabi, Said Ahmed Mohamed Khamis, Shafi Adam Shafi na M.S. Mohamed.

Utanzu wa tatu wa Fasihi Andishi ni tamthilia, utanzu huu pia hujulikana kama drama. Tamthilia ni fani ya fasihi iliyo na masimulizi yaliyokusudiwa kutendwa kwa hadhira jukwaani. Masimulizi ya tamthilia nyingi duniani na zile za Kiswahili zilizoandikwa zinasemekana kufuata muundo wa Tamthilia za Ki-Aristotle; mtiririko wa matukio wenye umbo la piramidi ambamo kuna chanzo, kukua kwa migogoro, kilele (cha hadithi/migogoro), na mshuko (kulegea kwa mvutano) na hatua ya mwisho ni suluhisho. Kwa maneno mengine, tamthilia hizo huwa na masimulizi yanayohusisha pande mbili zinazokinzana, na mgongano hukua na kufikia kilele na pindi mgogoro unaposuluhishwa, mchezo huwa umefikia tamati. Hata hivyo zipo tamthilia nyingi zinazofuata mtindo huo mathalan Mabepari wa Venisi ya William Shakespeare ambayo inaainishwa kama sanaa ya maonyesho na sifa zake ni pamoja na kuwapo na dhana inayotendeka, uwanja wa utendaji, watendaji, hadhira, kusudio la kisanaa, muktadha na ubunifu. Na tofauti na sanaa nyingine za maonyesho, msisitizo wa tamthilia upo katika matendo na mazungumzo ya wahusika. Waandishi wenye mchango wa kipekee katika Tamthilia Andishi ya Kiswahili ni pamoja na Ebrahim Hussein na Penina Mlama.

### 2.3 Chimbuko la Fasihi

Chimbuko la Fasihi ulimwenguni linahusishwa na nadharia kubwa nne; nadharia ya kidhanifu, nadharia ya sihiri, nadharia ya wigo, na nadharia ya kiyakinifu. Mulokozi (1996: 4-7) anabainisha na kuzihakiki nadharia hizo na hapa tutatolea muhtasari wake tu. Kwanza, ama kuhusu nadharia ya kidhanifu: Hii ni nadharia kongwe sana, nadharia hii inadai kuwa Mungu ndiye msanii mkuu na kuwa uwezo wa mwanadamu kubuni au hata mwanadamu mwenyewe ametokana na sanaa ya Mungu. Nadharia hii inachukulia uwepo wa sanaa tangu mwanzo wa mwanadamu, lakini dosari yake ni uchanganyaji wa imani na taaluma ya fasihi na kupuuza

athari ya mazingira katika harakati za mtu na uundaji wa utamaduni wake.

Mtazamo wa pili juu ya chimbuko la Fasihi ni nadharia inayodai kuwa Fasihi inatokana na imani ya sihiri; nguvu za kimiujiza (magic) katika juhudi za mwanadamu kukabiliana na kuyadhibiti (kuyashinda) mazingira yake. Mlokozi (kashatajwa) anafafanua kwa kutolea mfano wa wawindaji ambao wanaamini wanaweza kufanikiwa katika uwindaji kwa kutanguliza kuichora picha ya mnyama, kuichoma mkuki wakiamini sihiri; kuwa kwa kufanya hivyo kutaleta matokeo wanayotarajia (kufanikiwa kupata/kumwinda mnyama). Pia, anaeleza kuwa maneno na nyimbo walizonuizia ndiyo dalili ya ushairi wa mwanzo. Naye mwandishi anakosoa nadharia hiyo kama haitusaidii sana kujua chimbuko la fasihi kwani inachanganya chimbuko na dhima, na kuwa sihiri ni amali mojawapo tu miongoni mwa amali nyingi ambazo kwazo mwanadamu alitumia fasihi au sanaa.

Mtazamo wa tatu unahusu nadharia ya wigo (mimesis) nayo inadai kuwa mwanadamu alianza ubunifu wake kwa kusawiri maumbile yaliyomzunguka tu kama vile miti, wanyama, ndege, watu n.k. Na kuwa uigaji huo hauwezi kuwa na uhalisi, kwani unaiga maumbile na maumbile hayo yanaiga tu kazi ya Mungu. Mlokozi (kashatajwa) anaeleza kasoro ya nadharia hii kama imeegemea sana katika mwigo na kusahau kipengele cha ubunifu, ambacho kama kisingekuwapo katika fasihi basi kazi hizo zingetuchusha na kupwaya sana.

Nadharia ya nne ni ile inayofafanua kwamba Fasihi ni zao la mabadiliko katika maisha ya mwandamu kutoka unyama hadi hali ya utu na kuwa Fasihi ilitumika kama chombo cha mawasiliano katika uzalishaji mali na kuwa kadiri mwanadamu alivyomudu kukabiliana na mazingira yake, Fasihi ilijengeka kama sanaa ya burudani au ya shughuli maalumu za kijamii k.v sherehe na ibada. Nadharia hii ya uyakinifu ndiyo inayoelekea kukubalika zaidi kitaaluma kuliko zile na wigo na za kidhanifu ukiacha dosari ya maelezo yake juu ya mabadiliko ya mwanadamu kutoka hali ya unyama hadi utu, maelezo ambayo bado hayajathibitika kikamilifu na kuwa ugunduzi na ushahidi wa kisayansi na kiakiolojia bado unaendelea kukusanywa.

Kwa kukamilisha sehemu hii kuhusiana na chimbuko la Fasihi tunaweza kusema kwamba nadharia inayooelekea kukubalika kuhusiana na Chimbuko la Fasihi ni ile yenye mtazamo wa kiyakinifu, kwamba fasihi ni matokeo ya mapambano ya mwanadamu na mazingira yake, akiitumia fasihi kama njia ya mawasiliano na kuibua hisia na kuwa kadiri mwanadamu alivyoendelea kukabiliana na kuyamudu mazingira yake ya kimaumbile na kijamii ndivyo sanaa yake ilivyozidi kupevuka na kukomaa.

## 2.4 Dhima ya Fasihi

Dhima ya fasihi imepata kuhakikiwa na wataalamu mbalimbali ulimwenguni. Mwanafalsafa Aristotle, anatoa dhima tatu za fasihi; kuburudisha, kujenga tabia na kustarehesha (Mulokozi 1996:10-11). Mulokozi (kashatajwa) anaendelea kubainisha matapo mawili ya wahakiki wa fasihi wa Ulaya waliokuja baada ya Aristotle; kundi la kwanza na lililokuwa na wafuasi wengi likidai fasihi ni sanaa tamu na yenye dhima muhimu katika jamii. Dhima zilizotajwa sana ni pamoja na kuburudisha, kuelimisha, kujenga tabia, kuonyesha ukweli wa maisha, kuhifadhi lugha kuendeleza harakati za jamii na kujenga utaifa. Miongoni mwa wahakiki wa kundi hili ni

Horace (65-8 kabla ya Masihi) ambaye anajulikana kama muasisi wa kauli kuwa fasihi ni "sanaa tamu na tumizi" na aliyekuwa mhakiki wa kale wa Kirumi na wengineo waliokuja baadaye kama vile Sir Philip Sidney (1154 - 1586) na Alexander Pope (1638-1744). Mtazamo huu ulikuja kuendelezwa na wahakiki wa Kimarx katika karne ya 19 na 20.

Tapo la pili ni la wale waliodai kuwa msingi wa sanaa ni ujumi (kanuni za uzuri au ubaya wa kazi za sanaa) tu, sanaa haifai kufungamanishwa na vipengele vilivyo nje ya sanaa k.v dini au siasa, "sanaa ni kwa ajili ya sanaa tu". Na kwa mtazamo wa kundi hili sanaa haina dhima ya kijamii. Waasisi wa mtazamo huu wanatajwa kuwa wanafalsafa wa Udachi hususan Immanuel Kant (1724- 1804), na baadaye kuungwa mkono katika kazi za wananadharia kutoka Ufaransa kama T. Gautier katika dibaji ya riwaya yake Mademoiselle de Maupin ya mwaka 1935, na kazi za watunzi kutoka Marekani hasa Edgar Alan Poe katika makala yake ya "The Poetic Principle" ya mwaka 1850 (Mlokozi 1996: 11). Hata hivyo Mulokozi (kashatajwa) anabainisha kuwa katika muktadha wa Fasihi ya Kiswahili mtazamo huu haujawahi kuungwa mkono. Na kuwa wahakiki wengi wa Fasihi ya Kiswahili wakiwemo Kezilahabi (1980), Sengo na Kiango (1973 na 1974), Mulokozi (1973) na Senkoro (hakuna tarehe iliyotajwa) wanakubaliana na dhima ya Fasihi kama zilivyoainishwa na wahakiki wa Ulaya isipokuwa ile ya "sanaa kwa ajili ya sanaa tu".

Pia Mulokozi (kashatajwa juu) kwa kuzingatia mawazo ya wahakiki mbalimbali wa Fasihi ya Kiswahili, na kuzingatia dhana ya tabaka (mgawanyo wa makundi ya watu kulingana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia za uzalishaji mali) na itikadi (mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au kijamii) anazigawanya dhima za Fasihi katika makundi makuu matano; Dhima ya Kiitikadi, Kiuchumi, Kitamaduni, Kisiasa na Kifalsafa. Na sasa tutatolea ufafanuzi dhima hizo tano japo kwa muhtasari.

Dhima ya fasihi Kiitikadi kwa kifupi inarejelea msimamo wa mtunzi wa kazi ya fasihi katika jamii/muktadha wa wakati huo. Fasihi kwa mantiki hiyo inaweza kuwa upanga wenye ncha mbili ama ikashika dhima ya kutetea tabaka tawala au ikaipinga na kutetea itikadi ya watawaliwa. Mashairi ya Saadani Kandoro kama vile; "Siafu Wamekazana", "Kwetu ni Kwao kwa Nini? na "Ondoka nchini Mwetu" yanatolewa kama mfano wa kazi za fasihi yenye dhima ya kiitikadi na inayopinga ukoloni na kudai uhuru. Mashairi hayo yanangukia katika kundi la utetezi wa tabaka la wanyonge/watawaliwa.

Ama kwa upande wa dhima ya Kiuchumi; hii inahusishwa zaidi na Fasihi Simulizi. Mfano mzuri ni nyimbo za kazi zinazokusudiwa kuwatia nguvu na hamasa watu wakati wa uzalishaji. Pia mwandishi huyo anabainisha kuwa katika uchumi wa kisasa kwa upande mmoja, Fasihi ina dhima kubwa mbili; kuwaliwaza watu baada ya kazi na kuwapumbuza watu kutokana na heka heka na changamoto za maisha. Kwa upande mwingine katika jamii za kisasa Fasihi ni bidhaa na njia ya kujipatia kipato, watunzi, wachapishaji, na wauzaji wa vitabu wanaweza kunufaika na kazi za kifasihi kama michezo ya kuigiza/ sinema na riwaya.

Kitamaduni, fasihi inatajwa kuwa na dhima mbalimbali na hapa tutazidondoa mbili ambazo zina uzito zaidi kulingana na mwelekeo wa makala hii nazo ni; kuhifadhi na kurithisha amali za jamii, na kudumisha na kuendeleza lugha. Amali za jamii ni pamoja na mila, desturi, mtindo wa maisha, imani, historia, visasili, visakale, maarifa ya jadi (k.v. tiba, kilimo, uwindaji,

ufundi) na kadhalika. Tamthilia ya Kinjekitile iliyoandikwa na Ebrahim Hussein (1969), riwaya iitwayo Kurwa na Doto ya mwandishi Farsy (1960) na riwaya ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka iliyoandikwa na Kitereza (1980) ni mifano ya kazi zinazohifadhi na kuonyesha mila na desturi za jamii zinazoakisiwa humo. Kwa upande wa dhima ya kuendeleza lugha; kama tulivyosema katika utangulizi wetu fasihi ina uzito na nafasi muhimu na ya kipekee katika jamii (ukilinganisha na sanaa zingine) kwani nyenzo yake kuu ni lugha. Na kadiri watunzi wanavyoitumia na kuisuka lugha kiufundi katika kazi zao ndivyo inavyozidi kukua na kupevuka. Mathalan, inasemekana kuwa washairi walitumia maneno magumu au yasiyokuwa ya kawaida na hivyo kuwa ghala ya kuyahifadhi maneno hayo yasipotee katika matumizi.

Hatimaye tutajumuisha dhima ya Fasihi Kisiasa na ile ya Kifalsafa. Kisiasa, fasihi imekuwa na mchango muhimu katika harakati mbalimbali za kisiasa kote ulimwenguni na katika vipindi mbambali vya kihistoria. Mfano nchini Tanzania tuna mifano ya nyimbo zilizotumika wakati wa kudai uhuru, nyimbo za kutetea siasa ya chama tawala baada ya Uhuru, nyimbo mashuhuri kama vile "Tanzania Tanzania" wimbo wa taifa wenye kuhimiza uzalendo. Ama Kifalsafa, baadhi ya kazi za fasihi hujaribu kueleza au tuseme kujibu maswali mazito kuhusiana na falsafa ya maisha kama vile juu ya uwepo wa mwandamu duniani na mwisho wake. Mulokozi (kashatajwa) anatolea mfano wa kazi ya Utenzi wa Inkishafi uliondikwa na Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir (1972) kama maandishi ya kifalsafa katika Fasihi ya Kiswahili. Kazi nyingine ni kama riwaya za Euphrase Kezilahabi hasa Nagona (1987), riwaya ya M.S. Mohamed iitwayo KIU (ya mwaka 1972) na mashairi mengi ya mwandishi mashuhuri wa Kiswahili, Shaaban Robert.

## 3. Sanaa

Katika Sehemu hii tutaanza na fasili ya dhana Sanaa na kubainisha vipengele vya sanaa kwa ujumla kisha. Kisha tutabainisha vipengele teule vya Sanaa katika Utamaduni wa Kiswahili na kuvitolea maelezo na mifano ya sanaa mahsusi katika kila kipengele sambamba na dhima au kazi za sanaa husika. Vipengele vilivyoteuliwa ni pamoja na Ususi, Uchoraji, na Uchongaji.

### 3.1 Sanaa ni nini?

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili, Sanaa ni ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro, maigizo, nyimbo au uchongaji, au zao linalotokana na ufundi huo (KKS 2019:562). Pia tunaweza kufasili sanaa kama ufundi anaoutumia mwanadamu ili kuwasilisha fikra au mawazo yaliyomo akilini mwake. Sifa kubwa ya sanaa ni uzuri unaoonekana katika umbo lililosanifiwa kwa lengo la kuibua hisia au kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Ama kwa hakika kazi za sanaa ni pamoja na fasihi, ususi, uchoraji, uchongaji, ufinyanzi, muziki, ujenzi, na kadhalika. Kila umbo huwa na nyenzo kuu inayobeba umbo la sanaa husika. Ingawa fasihi ni moja ya sanaa, sanaa hiyo inajipambanua na kutofautiana na sanaa nyingine kwa matumizi yake ya lugha kama nyenzo na malighafi kuu katika kuunda na kuifikisha fasihi kwa hadhira yake. Na tumeijadilili sanaa hiyo (fasihi) kwa kirefu kidogo katika sehemu iliyotangulia. Katika sehemu ifuatayo, tunateua baadhi tu ya sanaa

nyinginezo na kuzitolea maelezo ikiwemo sifa na matumizi ya kila moja katika muktadha wa utamaduni wa Kiswahili.

### 3.2 Vipengele Teule vya Sanaa katika Utamaduni wa Kiswahili

Sehemu ifuatayo inatolea ufafanuzi, mifano na dhima ya vipengele teule vya sanaa hususan sanaa za kazi za mikono katika utamaduni wa Kiswahili.

#### 3.2.1 Ususi

Kwanza tutambulisha mikeka; mkeka ni jamvi lililosukwa kwa kili zinazoweza kunakshiwa kwa rangi na zenye umbo la mraba au mstatili na ukubwa wa aina mbalimbali. Kwa wastani kila nyumba ya Kiswahili haikosi mkeka kwani ni sanaa tumizi katika maisha ya watu ya kila siku. Kwa kawaida mkeka hutandikwa chini na watu wakakalia ndani ya nyumba, uani mathalan wakati wa mlo, jamvini pia ni mahali pa kukaribishia wageni aghalabu nje ya nyumba/ uani. Vile vile jamvini ni pahala pa kupumzikia, kufanya mazungumzo na jamaa na marafiki, pahala pa kuswalia kwa waislamu au hata pa kina mama kukaa na kusukana. Aidha, mikeka hutumika wakati wa shughuli za kijamii kama harusi, maulidini na misibani wakati wa kulala matanga. Pili ni Vikapu: Vikapu ni mfano wa sanaa nyingine inayotokana na kusuka kili na kupata kifaa/chombo chenye matumizi mengi katika maisha ya kila siku. Vikapu kitamaduni hutumika kwendea sokoni (kununua mahitaji ya chakula), katika shughuli za uvuvi, kubebea vitu n.k. Tatu, tuangalie ususi wa Nywele: ususi wa nywele ni sanaa na urembo hususan kwa wasichana. Ususi wa nywele huwa ni sehemu ya utunzaji wa nywele za Kiafrika kwa ujumla na una mitindo mashuhuri mbalimbali k.v. twende kilioni (mtindo wa kusuka mistari inayoelekea nyuma), vitunguu au mabutu (mtindo wenye umbo mfano wa kitunguu), kilimanjaro (mtindo wa kusuka mistari inayokutana kati kati ya kichwa na kufanya umbo mfano wa kilima), mdomo wa kuku/ jicho la mke mwenza (mtindo wa kusuka mistari kwa kuanzia katika pembe mojawapo ya kichwa agh. karibu na sikio yenye umbo mfano wa mdomo wa kuku. Aidha kama tulivyokwisha sema kusuka nywele ni urembo kwa wasichana lakini si adabu kwa vijana wa kiume kusuka nywele kwani hivyo ni sawa na kujifananisha wa watoto wa kike. Nne: Nyungo: ungo ni chombo kama sinia kilichotengenezwa kwa kupishanisha chale za miwale. Nyungo huweza kunakshiwa pia kwa rangi, na ni kifaa muhimu cha matumizi ya kila siku nyumbani kwani hutumika kupeta, kuchambulia nafaka kama mchele, kuwekea /kubebea mahitaji wakati wa mapishi, kuanikia vitu kama mihogo juani n.k. Tano; ni sanaa ya Kawa na Vipepeo: Kawa na vipepeo pia husukwa kwa kili na kunakshiwa kwa rangi nazo zina matumizi katika maisha ya kila siku. Mathalan Kawa hutumika kufunikia chakula na kipepeo hutumika kujipepea kwa joto au ishara ya mapenzi kwa mke anapompepea mumewe. Hata hivyo sanaa hizi mbili zina sifa ya ziada, kitamaduni kawa na vipepeo huwa na misemo kama vile; “Karibuni Wageni” “Funika Vifunikike Mlaji Afurahike” au “kipepeo si feni ni mapenzi.” Misemo ya Kawa na Vipepeo ni ya kisanii na kama ilivyo kwa misemo ya kanga katika utamaduni wa Kiswahili misemo hiyo ni chombo madhubuti cha mawasiliano au kufikisha ujumbe. Maana ya Kawa na maana ya ishara zinazotumika katika Kawa hususan katika jamii ya Wazanzibari imejadiliwa kwa kina na

Makallo, 2019 (604-616) kupitia nadharia ya kisemiotiki, naye anabainisha kuwa misemo hiyo inaakisi busara, hekima na maadili ya Wazanzibari na kuwa Kawa ni chombo kinachosetiri na kuhifadhi utamaduni wa jamii husika.

### 3.2.2 Uchoraji

Hapa tutaangalia mifano ya sanaa mbili nazo ni uchoraji wa Hina na uchoraji wa Picha. Tukianza na Uchoraji Hina: Hina ni majani yatokanayo na mti wa hina, na majani hayo aghalabu hukaushwa, yakapondwa na kuwa unga, kisha kuchanganywa na chai ya rangi (maji na majani ya chai) na wengine hutia ndimu na kupata uji uji mzito kiasi ambao hupakwa katika kucha au kuchorwa katika ngozi. Rangi inayotoka katika hina na kubakia katika kucha au ngozi ni kama kahawia au damu ya mzee hivi. Hina ni urembo wa kitamaduni hususan urembo wa wanawake. Kwa Waswahili hina huongeza nakshi na mvuto kwa mwanamke na kitamaduni hasa haifai kwa mwanamke kwenda majiani akionyesha urembo wa hina kwa wanaume wasiomhusu. Hina hupakwa wakati wa sherehe kama Harusi na Iddi. Hina inaweza kukaa wiki kadhaa katika ngozi/kucha. Inasemekana kama hina asilia (ambayo haijaongezwa kemikali) ina uwezo wa kuimarisha kucha na nywele. Wanaume hupaka katika nywele au ndevu hususan kubadili rangi ya mvi.

Sanaa nyingine katika kategoria hii ni Uchoraji wa Picha: Hizi huchorwa katika karatasi, ubao au kitambaa kwa kawaida. Maudhui ya picha huakisi maisha ya kila siku ya watu pamoja na kuonyesha mazingira yao. Mathalani picha inaweza kuonyesha majengo ya makazi kama nyumba za makuti, au watu wakiwa wamekaa nje ya nyumba, chini ya mti, kuzunguka moto, wakifanya mazungumzo au kucheza michezo kama bao. Vile picha huweza kuakisi mandhari ya pwani, baharini, vyombo vya baharini, shughuli za uvuvi, milima, wanyama, na miji ya kihistoria. Picha za Tingatinga hususan na zile zinazoakisi watu wa jamii ya kimasai na wananyama wapatikanao katika hifadhi za wanayama pori kama Serengeti ni maarufu kwa watalii wanaotembelea Tanzania.

### 3.2.3 Uchongaji

Uchongaji unarejelea sanaa na vifaa au bidhaa zinazotengenezwa kwa mikono, malighafi muhimu ikiwa ni mbao ambazo huchongwa kwa kisu. Sanaa ya uchongaji hutupatia vitu vya kidesturi na vyenye kazi katika maisha ya kila siku ya katika jamii za Kiswahili. Kutoka sasa tutatolea mifano ya vifaa hivyo na sifa au kazi zake. Mosi ni Mbuzi: Mbuzi ni kifaa cha kukunia nazi jikoni, kwa desturi Waswahili hutumia nazi katika mapishi yao kama vile wali wa nazi au mchuzi, na vitafunwa kama vibibi vitengenezwavyo kwa mchele basi mbuzi ni kifaa kisichokosekana katika jiko la Mswahili. Pili, Kinu: Kinu kidogo hutumika kutwangia viungo kama tangawizi, hiliki n.k katika mapishi. Kinu kikubwa aghalabu kutwangia nafaka kama mahindi. Tatu, tutafafanua kigoda: Hiki ni kiti cha mbao chenye miguu mitatu kwa kawaida na hutumiwa na akina mama jikoni. Ni desturi katika sehemu nyingi Afrika kupikia jiko la kuni au mkaa na mpishi hukaa kitako katika kigoda wakati wa mapishi. Nne ni Vinyago, hivi husawiri wanyama wapatikanao mbugani hasa wanayama kama vile; simba, nyati, tembo, chui, twiga, kifaru n.k. Pia taswira za watu maarufu kama aliyekuwa rais wa kwanza wa Tanzania

na Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, rais wa zamani wa Afrika Kusini hayati Nelson Mandela, Rais mstaafu wa Marekani Barack Obama na wengineo. Katika kundi hili, vinyago vya Kimakonde ni maarufu zaidi hasa miongoni mwa watalii wao hupenda kuzinunua na kuzibeba na kurejea nazo makwao kama kumbukumbu wanapotembelea mahali kama Tanzania ili kuona wanyama pori. Maudhui ya vinyago vya kimakonde ni kama vile vinavyoashiria falsafa ya ujamaa (ambayo huwasilishwa kwa taswira ya watu wengi walioshikamana) na kuakisi taswira na watu wa jamii ya Kimasai na shughuli zao. Vifaa vingine vinavyotokana na sanaa hii ya uchongaji ni pamoja na chanuo au shanuo: hiki ni kitana kikubwa kilichotengenezwa kwa mti cha kuchania na kusukia nywele kwa wasichana au kina mama. Nacho kinaweza kupambwa kwa nakshi za michoro. Sanaa ya uchongaji pia inahusisha utengenezaji wa zana za kupikia jikoni kama vile mwiko, upawa. Aidha kila zana katika fani hii ya uchongaji huchongwa kwa ustadi mkubwa ikiwa na mvuto ukiachilia mbali uwezo wa kutumika katika matumzi ya kila siku.

## 4. Hitimisho

Kila jamii ina fasihi yake ambayo watu wake wanajivunia kama sehemu ya utamaduni na utambulisho wao na viwili hivi; Fasihi na Jamii (au utamaduni wa jamii inamotoka fasihi husika) ni kama pande mbili za sarafu moja, hatuwezi kuvitenganisha. Fasihi inasawiri, na kuhakiki maisha ya jamii husika. Makala hii basi imetalii na kutolea ufafanuzi mambo ya msingi kuhusiana na **Fasihi ya Kiswahili** na kuelezea vipengele teule vya **Sanaa** vinavyofungamana na Utamaduni wa Kiswahili sambamba na kufahamisha dhima zake. Makala hii imetangulia kwa kufafanua dhana ya fasihi kwa ujumla, ikifuatiwa na dhima za vipengele vya fasihi ya Kiswahili. Pia tumetolea ufafanuzi kuhusu sanaa kwa ujumla na kisha kuelezea kazi au dhima ya vipengele teule vya sanaa katika utamaduni husika.

Ni matumaini ya mwandishi kuwa makala hii italeta natija katika kukidhi mahitaji ya rejea za msingi zilizolengwa kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Makala hii ni sehemu ya mfululizo wa makala tano zilizotangulia zilizokusudiwa kwa kundi tajwa zenye kuangazia na kufafanua vipengele mbalimbali vya Utamaduni wa Kiswahili. Makala zilizotangulia katika mfululizo huu ni pamoja na; Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamduni wa Kiswahili (Isack 2018:105-118), Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili (Isack 2019:259-269), Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi (Isack 2020:193-205) na Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili (Isack 2021:223-233), na Utamaduni wa Kiswahili: Misingi ya Lugha (Isack 2022: 247-258).

Vipengele vinavyoutambulisha utamaduni wa watu ni vingi na anwai kwani Utamaduni ni jumla ya maisha ya watu. Hapa tutadondoa japo kwa muhtasari vipengele vilivyozungumziwa katika makala tano zilizotangulia zenye mwelekeo na azma moja na makala ya sasa. Makala ya kwanza, inatalii Mila za Makuzi na Hatua za Maisha yaani kutoka kuzaliwa mpaka kifo. Hatua na mila hizo ni pamoja na zile za mazazi, makuzi (balehe), ndoa na harusi na zile zinazohusiana na misiba/kifo. Makala ya pili, ni masuala ya Familia na Unasaba hususan dhima za makundi mbalimbali ya watu katika familia k.v wazazi, watoto, wanaume, wanawake na ndugu na jamaa

wengine. Katika mada hii pia methali zinazogusia mambo ya familia zimechambuliwa. Makala ya tatu inaelezea masuala ya Dini na Imani nyingine (superstitions) ikiongozwa na hoja ya kuwa maisha ya Waswahili kwa kiasi kikubwa yamefungamana na dini ya Kiislamu. Kwamba kwa Mswahili wa kweli dira ya maisha yake ni mafunzo na maamrisho ya dini yake, na hivyo basi hatuwezi kuuelezea utamaduni wa Waswahili vilivyo bila kugusia dini ya Kiislamu. Hata hivyo, makala hiyo inabainisha kuwa ijapokuwa Waswahili ni wafuasi wazuri wa dini ya Kiislamu, Waswahili wanazo imani nyingine zisizofungamana na dini hiyo. Makala ya nne, inahusu utamaduni wa Chakula, desturi za Mavazi, Adabu na Miiko ikijumuisha Ishara na lugha za mwili. Vyakula maarufu vya Kiswahili ni pamoja na wali, pilau na biriani. Kwa upande wa mavazi; kitamaduni mavazi yanagawanywa kwa kuzingatia jinsia, urasmi na heshima. Mavazi yanayofunika sehemu kubwa ya mwili hasa kwa wanawake ndiyo yanayotajwa kuwa ya heshima. Pia, Vazi la Khanga limepewa nafasi ya kipekee katika utamaduni wa mswahili, likiwa na matumizi anwai na yenye misemo (majina) inayotumika kama njia ya kufikisha ujumbe. Makala hiyo pia inafafanua mambo ya adabu na miiko, jambo ambalo ni muhimu sana kuzingatiwa ili kutangamana vyema na watu katika jamii yoyote ile iwayo. Makala ya tano katika mfululizo huo inaangazia Lugha ya Kiswahili ikiwemo historia, dhima yake zamani na leo na taaluma zake za msingi. Hatimaye katika makala hii tumeangazia zaidi juu ya Fasihi ya Kiswahili na Sanaa. Ni matumaini yetu kwamba makala hizi zimejumuisha vipengele au mada za msingi zinazoweza kumfaa mgeni yeyote mwenye hamu na raghba ya kujifunza Lugha hii adhimu ya Kiswahili na Utamaduni wake. Pia mada zilizotambulishwa katika makala hizi ni sehemu nzuri ya kuanzia kwa mtu mwenye hamu ya kuzamia zaidi katika nyanja za kitaaluma ikiwemo zile za kiisimu au za kifasihi za lugha ya Kiswahili.

## Marejeo

Ameir Issa Haji na wenzie

1981 Misingi ya Nadharia ya Fasihi, Kimetayarishwa na Kutolewa na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni/ Wizara ya Elimu Zanzibar- Tanzania, kimechapishwa na Berlings, Arlov, Sweden.

Isack, Zainabu Kassu

2018 “Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika Frontier of Foreign Language Education 1, 105-118.

2019 “Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika Frontier of Foreign Language Education 2, 259-269.

2020 “Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi”, katika Frontier of Foreign Language Education 3, 193-205.

2021 “Kaida na Miiko katika Utamaduni wa Kiswahili”, katika Frontier of Foreign Language Education 4, 223-233.

2022 “Utamaduni wa Kiswahili: Misingi ya Lugha” katika Frontier of Foreign Language Education 5, 247-258.

Makallo, Maimuna Ahmed
2019 "Uchambuzi wa Kisimiotiki wa Misemo ya kwenye Makawa ya Zanzibar", katika International Journal of Advanced Research (IJAR), Vol.7 (7), 604-616.

Mulokozi M.M
1996 Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii), Dar es Salaam, Tanzania

TATAKI
2019 Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 4), Oxford University Press, Nairobi, Kenya.